

# Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Pandemic EBT (P-EBT) ya Utunzaji wa Watoto

Mwaka wa Shule wa 2022-2023 (Tarehe 31 Machi 2023)

---

## Swali la 1: P-EBT ya Utunzaji wa Watoto ni nini?

Jibu: Ni msaada wa chakula wa muda ulioidhinishwa na serikali ya shirikisho kusaidia familia zilizo na watoto chini ya miaka 6 wakati wa janga la COVID-19.

---

## Swali la 2: Ni nani anayestahiki kupata msaada wa P-EBT ya Utunzaji wa Watoto?

Jibu: Familia za Vermont zinazopokea msaada wa 3SquaresVT zilizo na watoto walio chini ya umri wa miaka sita. Msaada wa P-EBT wa utunzaji wa watoto utatolewa kila mwezi kuanzia Septemba 2022 hadi tarehe 11 Mei 2023 kwa familia zinazotimiza masharti. Msaada wa P-EBT wa utunzaji wa watoto utaisha tarehe 11 Mei kutokana na kuisha kwa dharura ya afya ya umma ya serikali ya shirikisho.

---

## Swali la 3: Msaada wa P-EBT wa Utunzaji wa Watoto ni kiasi gani?

Jibu: Msaada wa P-EBT wa utunzaji wa watoto ni wa kiasi cha \$34.79 kwa kila mtoto kwa mwezi kwa Septemba 2022 hadi Januari 2023. Kiasi cha Februari hadi tarehe 11 Mei bado hakijabainishwa. Kiasi cha msaada wa utunzaji wa watoto cha mwezi Mei kitakuwa kiasi kilichokadiriwa kwa sababu msaada unaisha katikati ya mwezi huo.

---

## Swali la 4: Kuna msaada wa P-EBT wa Utunzaji wa Watoto wa Msimu wa Kiangazi?

Jibu: Kwa sababu dharura ya afya ya umma ya serikali ya shirikisho imeratibiwa kuisha tarehe 11 Mei, hakutakuwa na msaada wa P-EBT wa utunzaji wa watoto wa msimu wa kiangazi. Sheria ya shirikisho hairuhusu Vermont kutoa msaada wa P-EBT wa utunzaji wa watoto wa msimu wa kiangazi wakati hali ya dharura ya afya ya umma imekwisha.

---

## Swali la 5: Je, msaada wa P-EBT wa Utunzaji wa Watoto utatumwa lini?

Jibu: Msaada wa duru ya kwanza (kwa Septemba 2022 hadi Januari 2023) utatumwa katika mwezi wa Aprili 2023. Watoto wanaotimiza masharti ya msaada wa P-EBT wa Utunzaji wa Watoto watapokea malipo moja kwa miezi ya msaada ya Septemba hadi Januari kwa kila mwezi ambao familia ilipokea msaada wa 3SquaresVT.

Msaada wa miezi ya Februari hadi tarehe 11 Mei imepangwa kutumwa mwishoni mwa Agosti.

---

## Swali la 6: Je, nitajuaje kama familia yangu inastahiki msaada?

Jibu: Economic Services Division (ESD, Kitengo cha Huduma za Kiuchumi) itabaini ikiwa mtoto wako anastahiki, kulingana na vigezo vilivyo hapo juu. Ikiwa unastahiki, utapata barua kutoka kwa ESD inayoeleza jinsi na lini utapokea msaada.

---

**Swali la 7: Kama tunastahiki, tutapokeaje msaada huu?**

Jibu: Msaada wa P-EBT wa Utunzaji wa Watoto hutumwa kwenye kadi ya EBT iliyotolewa kwa familia yako kwa msaada wako wa 3SquaresVT.

---

**Swali la 8: Malezi ya mwanafunzi wangu yamegawanywa kati ya familia mbili. Ni familia gani itapokea msaada?**

Jibu: Msaada utatumwa kwa mtu mzima ambaye ameorodheshwa na ESD kama mkuu wa familia katika msaada wa 3SquaresVT.

---

**Swali la 9: Ni bidhaa gani ninazoweza kununua na msaada huu?**

Jibu: Angalia [orodha ya bidhaa zinazoruhusiwa za vyakula](#) kwenye tovuti ya USDA.

---

**Swali la 10: Ni maduka gani ninayoweza kutumia kadi yangu ya P-EBT?**

Jibu: Unaweza kuitumia kununua vyakula katika duka lolote linalokubali 3SquaresVT. Hizi ni pamoja na maduka ya vyakula, maduka makubwa, maduka ya karibu na masoko mengi ya wakulima katika Vermont. Pata maelezo zaidi kwenye [ukurasa wa tovuti wa EBT wa DCF](#).

---

**Swali la 11: Sina watoto wowote wanaoenda kwa huduma ya utunzaji wa watoto. Naweza kupata msaada huu?**

Jibu: Ndiyo. Watoto wote walio chini ya umri wa miaka sita na wanaopokea 3SquaresVT wanastahiki kupata msaada huu.

---

**Swali la 12: Nina watoto wengine wenye umri zaidi ya miaka sita. Je, wanastahiki kupata msaada wa P-EBT wa utunzaji wa watoto?**

Jibu: Hapana. Msaada huu unatolewa tu kwa watoto wanaopokea 3SquaresVT ambao wako chini ya umri wa miaka sita. Tafadhali angalia Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu P-EBT ya Shule kwa maelezo zaidi kuhusu msaada unaopatikana kwa watoto walio na umri wa kwenda shule.

---

**Swali la 13: Itakuwaje ikiwa sitaki msaada huu?**

Jibu: Ni hiari kushiriki. Ikiwa hutaki kushiriki, usitumie msaada wa ziada unaotumwa kwenye kadi yako EBT ya 3SquaresVT.

---

**Swali la 14: Je, msaada wa P-EBT utaisha ikiwa hautatumika?**

Jibu: Ndiyo. Muda wa msaada wa P-EBT utakwisha ikiwa kadi haitatumika ndani ya siku 274.

---

**Swali la 15: Nina maswali zaidi. Ninaweza kupata wapi maelezo zaidi?**

Jibu: Nenda kwenye <https://dcf.vermont.gov/esd/P-EBT> au piga simu 1-800-479-6151, chaguo la 7, kwa maelezo zaidi.